


Misingi ya Hifadhi ya Jamii: Sera ya uchumi inayofaa

Kuendelea na utekelezaji wa Misingi ya Hifadhi ya Jamii kunachangia katika ukuaji endelevu wa kiuchumi kwa kukuza uzalishaji wa ajira, kuwawezesha watu kupata kazi zenye staha, kuimarisha mahitaji ya jumla na kuimarisha uchumi wa ndani.




Shirika la Kazi Duniani (ILO) linavyosaidia nchi mbalimbali kujenga misingi ya hifadhi ya jamii

Kwa kupitia programu yake ya kimataifa na huduma za ushauri wa kitaalamu, Shirika:

- linatoa misaada ya kitaalamu ya kuandaa, kukadiria gharama na kutekeleza mifumo ya hifadhi ya jamii
- linahimiza majadiliano jumuishi ya kijamii kitaifa kuhusu utoaji wa hifadhi ya jamii
- linatetea uundaji wa Misingi ya Hifadhi ya Jamii iliyofasiliwa kitaifa kwa wote na kuongeza mifumo ya kitaifa ya hifadhi ya jamii
- linahimiza ipasavyo kuridhia Mkataba wa Hifadhi ya Kijamii (Viwango vya Chini), (Na. 102) na viwango vingine vilivyo bora zaidi
- linaandaa na kusambaza ujuzi.

Shirika linashirikiana kupitia muungano wa uongozi wa Umoja wa Mataifa na juhudi za pamoja za Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile - Bodi ya Ushirikiano ya Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya Hifadhi ya jamii, inayongozwa kwa pamoja na ILO na Benki ya Dunia (WB).

Shirika limetoa katika miaka ya hivi karibuni misaada ya kitaalamu kuhusu hifadhi ya jamii kwa nchi zaidi ya 135



Kitu gani kinafuata?

Sasa ni wakati wa kuchukua hatua!

Nchi 184 kuanzisha misingi ya hifadhi ya jamii na kuweka mikakati ya kutoa hifadhi ya jamii kupitia majadiliano ya kitaifa. Ili kufanikisha hili:


- Zitapanga malengo kulingana na vipaumbele vya nchi
- Zitabainisha mapengo na vikwazo katika hifadhi ya jamii
- Zitaandaa mifuko sahihi na inayoratibiwa
- Zitaunganisha hifadhi ya jamii kitaifa na sera za soko la ajira
- Zitatathmini gharama, zitabainisha rasilimali zinazohitajika na kuweka mipango endelevu ya baadaye
- Zitaamsha ufahamu kuhusu hifadhi ya jamii.

Nchi nyingi zimeendelea vya kutosha, zimekuwa zikitoa huduma ya hifadhi ya jamii kwenye muongo uliopita. Zinatoa ushahidi mzuri zaidi kuwa uundaji wa misingi ya hifadhi ya jamii utafikiwa.

“Katika hali isiyoieleweka ya mabadiliko duniani na mahitaji kidogo, uanzishaji wa Misingi ya Hifadhi ya Jamii ni fursa ya kusaidia kuimarisha uchumi, kujenga ukua-ji wa uchumi jumuishi, na kujenga uimara wa kisiasa. Misingi ya Hifadhi ya Jamii ni zana muhimu ya kuzisaidia nchi kupunguza umaskini, kuzuia tofauti za usawa, kuimarisha unyumbukaji, na kuweka msingi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya binadamu.”

Wito wa pamoja wa Helen Clark, Mwenyekiti wa UNDG/Mtawala UNDP na Guy Ryder, Mkurugenzi Mkuu, ILO

www.social-protection.org
 Social Protection Platform
 @soc_protection



International
Labour
Organization

KUKUZA MISINGI YA HIFADHI YA JAMII KWA WATU WOTE
HUU NI WAKATI WA KUCHUKUA HATUA



« Hifadhi ya jamii kwa wakati huu inapaswa kuwa haki ya binadamu na sera ya uchumi inayofaa »
 Guy Ryder, Mkurugenzi Mkuu, ILO

Makubaliano yanayoibuka

Baada ya kukumbwa na umaskini uliokithiri na ongezeko la tofauti za usawa, makubaliano yameibuka duniani kote kuhusu haja ya kutoa hifadhi ya jamii na kukuza ruwaza za ukuaji wa uchumi na maendeleo yanayojumuisha watu wengi zaidi.

Wawakilishi wa serikali, wafanyakazi na waajiri wa nchi wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) walipitisha kiwango kipya cha kimataifa mnamo mwaka 2012, yaani **Pendekezo la Misingi ya Hifadhi ya Jamii (Na. 202)**, mkabala ambao pia ulipitishwa na kundi la G20 na Umoja wa Mataifa.

Pendekezo la ILO ni wito mzito wa kuchukua hatua, kutoa mwongozo imara kuhusu kuunda misingi ya Hifadhi ya Jamii na kushughulikia mikakati ya utoaji wa hifadhi ya jamii. Linadhihirisha nafasi muhimu ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya maendeleo, ufufuaji wa uchumi, usawa zaidi na haki ya kijamii ndani ya utandawazi wa haki.

“Sihitaji kusubiri msaada kutoka kwa watu wengine”

Luísa Marques, mwenye umri wa miaka 81, ni mwananchi wa Cape Verde, anaishi katika jamii ya wavuvi pamoja na wajukuu zake. Luíssa ilimbidi azidi kutegemea misaada ya mara kwa mara kutoka familia yake. **“Maisha ni magumu, bahari mara nyingi haitabiriki na watoto wangu wamesaidia jinsi walivyoweza, lakini pia wana familia zao.”**

Mnamo mwaka 2011 Luísa alianza kupokea pensheni ya karibu Dola za Kimarekani 50 kwa mwezi. Mafao haya yameleta tofauti kubwa hasa katika maeneo ya vijijini na kwa wanawake. Wanawake wengi wa Cape Verde, licha ya kuwa wamefanya kazi maisha yao yote, hawakuwahi kupata kutambuliwa kihalali. **“Si malipo makubwa lakini yamebadili maisha yangu kwa sababu ninaweza kutegemea pensheni kununua mahitaji muhimu. Sihitaji kusubiri msaada kutoka kwa watu wengine.”**

Pensheni ya umma imekuwa ikilipwa tangu mwaka 2007, ikihusisha asilimia 74 ya wanawake wazee huko Cape Verde mwaka 2009, na inagharamiwa na malipo ya kodi kwa gharama ya asilimia 0.4 tu ya Jumla ya Pato la Ndani.

Misingi ya Hifadhi ya Jamii ni nini?

Misingi ya Hifadhi ya Jamii ni seti zilizopangwa kitaifa za angalau dhamana nne za hifadhi ya jamii ambazo zinahakikisha kuwepo kwa uhakika wa kipato kwa wote na upatikanaji wa huduma muhimu za afya kwa wote.

Zinapaswa kufafanuliwa kitaifa kupitia majadiliano muafaka ya kijamii na kuwawezesha watu kuishi maisha yanayojali utu. Zaidi ya hayo, dhamana zinapaswa kupangwa na sheria za kitaifa na utekelezaji wake unapaswa kufuatiliwa na kutathminiwa mara kwa mara.

Pendekezo la Misingi ya Hifadhi ya Jamii, 2012 (Na. 202) linahamasisha kuhusu madhumuni ya aina mbili:

- 1) Kupanga **Misingi ya hifadhi ya jamii kitaifa** katika msingi wa mifumo mipana ya hifadhi ya jamii.
- 2) Kuendelea kuhakikisha kuwepo **viwango vya juu vya hifadhi** vikiongozwa na Mkataba wa Hifadhi ya Jamii (Viwango vya Chini) (Na. 102) na viwango vingine vya ILO vya hifadhi ya jamii.

Misingi ya Hifadhi ya Jamii:

 Upatikanaji wa huduma za afya kwa wote	39%	ya watu duniani hawajajiunga na mfumo au mfuko wa huduma ya afya
	41%	ya jumla ya gharama za huduma ya afya inagharamiwa na kaya binafsi
	Kuna upungufu wa wafanyakazi milioni 10.3 wa huduma za afya duniani	
 Hifadhi ya jamii kwa watoto	50%	ya watoto duniani wanaishi katika hali ya umaskini
	0.4%	Asilimia 0.4 ya Jumla ya Zao la Ndani (GDP) hutengwa kwa wastani na serikali mbalimbali kwa ajili ya manufaa ya watoto na familia, lakini uwekezaji zaidi unahitajika
	Watoto 18,000 wanakufa kila siku kutokana na magonjwa ambayo mengi yanaweza kuzuiwa	
 Hifadhi ya jamii kwa watu wenye umri wa kufanya kazi	12%	ya wafanyakazi ambao hawajaajiriwa duniani wanapata mafao ya kutoajiriwa ipasavyo
	28%	ya wanawake wanapokea mafao ya uzazi kwa fedha taslimu
	39%	ya wafanyakazi huwa wanapata mafao yao yanayotokana na ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi
 Pensheni na huduma kwa wazee	49%	ya watu wenye umri wa kupata pensheni hawapati pensheni zao
	41%	ya wafanyakazi (umri wa miaka 15+) wanachangia katika mipango ya pensheni
	Wazee milioni 300 hawana uhakika wa kipato ili kuishi maisha bora	

Kwanini tunahitaji Misingi ya Hifadhi ya Jamii?

Hifadhi ya jamii ni sera muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu ambayo.....



Huendelea kuhakikisha kuwepo Misingi ya Hifadhi ya Jamii kwa wote